

Swahili transcript:

Daudi: Sasa mwenzangu wewe hapa Dar-es-salaama, mpaka sasa unafanya biashara gani?

Alimu: Mpaka sasa hivi biashara niliyoko nayo, ninayoendelea nayo, biashara, sasa hivi biashara ninayoendelea nayo ni kama biashara ya radio. Naenda kuchukua radio, napanga kwenye kimeza, nawasubiria watu kama wanakuwa wanahitaji wataakuja nita.. nitapata riziki.

Daudi: Mmmh.. sawa. Kwa hiyo hizo radio kwa kutwa nzima, kuianzia asubuhi mpaak jioni unaweza uu... ukuuza bei gani, kwa siku nzima?

Alimu: Kwa siku nzima, namshukuru mwenyezi Mungu, siku labda inaweza ikawa siku nzuri, kwa sababu siku zinafanana ila hazilingani. Kunasiku unaweza ukaenda kwenye goli ukajikuta unauhakika wa kuinziza elfu kumi na tano, elfu kumi na saba. Siku zingine ukaweza ukatoka na hukuingiza hata hela ya chai hujapata. Kwa siku unabidi uvumilie, siyo kwamba leo umekosa basi ukate tamaa, kwamba kabisa siku nzote nitakuwa nakosa kabisa. Hapana! Siku moja unapata siku nyingine unakosa.

Daudi: Ok! Kwa hiyo matumizi unayotumia kwa kutwa...labda matumizi madogo madogo nini kila kitu, huwa yanafikia bei gani kwa kutwa nzima?

Alimu: Mmh...matumizi madogo madogo si gharama kubwa sana na wala si yakutisha. Kwa sababu kunamatumizi kama ya maji, matumizi ya chakula, chai ya asubuhi labda matumizi ya usiku. Unaweza unajikuata gharama ina.. inagharimu kama kwenye elfu tatu au elfu mbili. Sasa ukijikuata kama umeingiza elfu kumi na tano kidogo unabaki na kiasi fulani chakuenze kuendeleza maisha yako ya baadaye.

Daudi: Kwahiyo wewe unaishi peke yako au una mke?

Alimu: Mimi naishi peke yangu mpaka sasa. Sijawahi kuoa hata siku moja.

Daudi: Kwa hiyo mpaka sasa wewe umeendeleaje katika hizo shughuli zako ndogo ndogo nini kila kitu? Kwa hiyo kunafaida au kuna hasara?

Alimu: Katika hizo shughuli, kwa kweli ninafurahi zaidi kwasababu sahivi hali ya sasa hivi, na hali niyokuwa nayo nyumbani, na hali niyonayo hapa mjini kwa kweli kiasi fulani, naweza kumshukuru mwenyezi Mungu. Hali niyokuwa nayo nyumbani nilikuwa na hali mbaya zaidi. Kwa hiyo sasa hivi hapa mjini kidogo nimeweza kubadilisha maisha, hata mwenendo unakuwa unaenda vizuri, najikuta mambo yangu yanakuwa mazuri. Nimechukua chumba. Kwahiyo vitu vya ndani kidogo alamdulilahi.

Daudi: Kwahiyo zinamanufaa sana?

Alimu: Manufaa yapo kiasi chake.

Daudi: Kwa hiyo ulianza na mtaji wa bei ghani?

Alimu: Msingi unategemea na kiasi ulichonacho. Ukiwa na elfu hamsini utaanza. Ukiwa kama na semanini, kama hela unayo kama laki moja unaweza ukaanzia au laki mbili kwa hiyo ni kulingana na kiasi ulichokuwanacho.

Daudi: Sawa. Kwa hiyo vipi na watu wa serikalini nini huwa hawafatili fuatili katika hizo biashara ndogo ndogo labda zenu mlizo nazo?

Alimu: Eeh..Watu wa serikalini huwa wanafuatilia, lakini inabidi uende nayo hivyo hivyo. Kunasiku wanaweza wakaja wakwa kwambia bwana inabidi unachie hela ya chai, usiponiachia hela ya chai nakuamisha. Aah inabidi unatoa. Unamwachia alfu, unamwachia mia tano. Siku nyingine unaweza kumaliza hata mwezi mzima na hawajakuja kuuliza. Kwa hiyo inakuwa unaenda nao tu hivyo hivyo tu hadi siku zineandelea kusogea.

Daudi: Kwa hiyo nyinyi mnalaiseni au mnanguvu kazi?

Alimu: Aghaaa...Hatuna laiseni wala nguvu kazi, maana biashara zetu ni biashara ndogo ndogo. Hauwezi ukaandaa nguvu kazi wala laiseni.

Daudi: Asante sana.

English translation:

Daudi: Now, my fellow citizen of Dar-Es-Salaam, until now, what kind of business are you in?

Alimu: The business I have run and continue to run is the business of selling radios and stereos. I take radios, arrange them on a table, and then I wait for customers who might need radios. They come and I will ...earn something.

Daudi: Mmmh... okay. So, in a whole day, from morning until evening, how much can you...sell?

Alimu: In a whole day, thanks to God, a day could be a good day, because the days look similar but they are not equal. For one day, I can make my goal and be certain that I will earn between 15,000 and 17,000 Tanzanian shillings. Then there are days you can set up for business and not even earn money for tea. So some days you just have to be patient, even if you didn't make anything for one day, even if you want to give up thinking that you won't make money ever again. No! Some days you make money, some days you don't make money.

Daudi: Okay! So, your expenses... As for your every day expense, how much money do you spend for a whole day?

Alimu: Mmmh...I don't spend a lot on a daily basis. This is because each day I simply buy water, food, breakfast and maybe dinner. So mostly, you find yourself spending around 2000 or 3000 Tanzanian shillings. So if you earned around 15,000, at least you will have some money left over for other things in the future.

Daudi: So, do you live by yourself or are you married?

Alimu: I live by myself until now. I never married.

Daudi: So, so far how are you doing in business? Do you make good money or is there not much of a profit?

Alimu: I like having this business because if you look at the life I live now compared to the life I lived at home (the country), the life I live here in the city is better, and I thank God for that. The life I lived at home was very bad. Therefore, now that I live in the city. I have changed my life and everything is going well. I have a room. I also have things in my room, *alamdulilahi*.

Daudi: So, there are advantages in doing the business?

Alimu: Yes! There are, to some extent.

Daudi: So, how much capital do you need to start out?

Alimu: It depends on how much money you have. If you have 50,000 Tanzanian shillings, you can start. If you have 100,000 or 200,000, you can start with that, it just depends on how much money you have.

Daudi: So, do the people who work for the government bother you about your business?

Alimu: Yes! They do but we just have to keep on going. Some days they might come and ask you to give them money for breakfast and if you don't give them anything they will move you. Aah... so we have to give them some money. We give them 1,000 to 5000 shillings. Sometimes you can be here for a month and they never show up. So you just keep on doing business as long as life goes on.

Daudi: So do you have a license or do you just need to be clever?

Alimu: Naaaahhh...We neither have a license nor do we need to be clever since our business is so small. We don't have to register our business and we don't need to be clever.

Daudi: Thank you.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated